JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

*Dodoma*
*11 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS DKT. SAMIA APOKEA UJUMBE MAALUM KUTOKA KWA KATIBU MKUU WA UMOJA WA MATAIFA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo tarehe 11 Machi, 2026 amepokea salamu za Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres, zilizowasilishwa kwake na Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bw. Parfait Onanga-Anyanga, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma.

Bw. Onanga-Anyanga yupo nchini Tanzania kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali na kutathmini hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha utulivu wa kisiasa, mshikamano wa kitaifa na kuendeleza misingi ya utawala wa sheria kufuatia matukio ya uvunjifu wa amani ya kabla na wakati wa Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba, 2025.

Mjumbe huyo maalum ameeleza kuwa Umoja wa Mataifa unatambua na kupongeza hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Tanzania baada ya matukio hayo, hususan uamuzi wa kuunda Tume Huru ya Uchunguzi, na dhamira ya kufanya mazungumzo jumuishi ya kitaifa, pamoja na kuendeleza mchakato wa mabadiliko ya kikatiba.

Ameongeza kuwa, Umoja wa Mataifa unaendelea kuitambua Tanzania kama nchi yenye historia ya muda mrefu ya amani, utulivu wa kisiasa na mshikamano wa kitaifa, pamoja na kuthamini mchango wake katika juhudi za kulinda na kuimarisha amani barani Afrika.

Katika ziara yake, Bw. Onanga-Anyanga amekutana na kuzungumza na viongozi wa taasisi mbalimbali nchini, ikiwemo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mahakama ya Tanzania, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, pamoja na viongozi wa vyama vya siasa.

Aidha, amekutana na kuzungumza na Mwenyekiti na wajumbe wa Tume Huru ya Uchunguzi pamoja na wadau wengine wa kisiasa na kijamii ili kupata maoni na mitazamo tofauti kuhusu masuala yaliyotokea na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali.

Bw. Onanga-Anyanga amesema mashauriano hayo yatauwezesha Umoja wa Mataifa kupata taswira halisi kuhusu uhalisia wa matukio ya tarehe 29 Oktoba, 2025, na juhudi zinazofanywa na Serikali ya Tanzania katika utatuzi wa changamoto zilizojitokeza wakati na baada ya matukio hayo, na kuongeza kuwa hatua hizo zina mchango muhimu katika kuimarisha maridhiano ya kitaifa, kurejesha imani ya wananchi na kuendelea kujenga taasisi imara za kidemokrasia nchini.

Halikadhalika, ameahidi kuwasilisha tathmini ya mashauriano hayo kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ili kuendelea kuimarisha mashauriano baina ya Umoja wa Mataifa na Tanzania.

Kwa upande wake, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuma salamu za shukrani na kupongeza hatua ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bw. António Guterres, ya kutuma ujumbe maalum nchini Tanzania ili kupata uelewa wa kina kuhusu hali ya nchi na kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali.

Rais Dkt. Samia amesema Serikali ya Tanzania imejizatiti kuhakikisha mchakato wa kufuatilia matukio hayo unafanyika kwa kuzingatia misingi ya utawala wa sheria, uwajibikaji na haki, huku ikiendelea kulinda amani, umoja wa kitaifa na utulivu wa kisiasa ambao umekuwa msingi wa wakati wote wa maendeleo ya nchi.

Aidha, ameeleza kuwa Serikali iko tayari kupokea na kuyafanyia kazi mapendekezo yatakayowasilishwa na Tume ya Uchunguzi mara baada ya kukamilika kwa kazi yake, akiongeza kuwa, mapendekezo hayo yatakuwa sehemu muhimu ya mchakato wa kuimarisha maridhiano ya kitaifa, pamoja na marekebisho ya Katiba.

Vilevile, amesisitiza kuwa Tanzania itaendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa na jumuiya za kimataifa katika kukuza demokrasia, utawala bora na maendeleo jumuishi.



Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu